

Haki za Kunakili Imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania

ISBN: 9987 – 620 – 01 – 3

Jina la Kitabu:	Muhimu wa Qur'ani
Muandishi:	Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi
Msafiri:	Sheikh Dhikiri U.M. Kiondo
Chapa:	Ya Kwanza 1998
Nakala:	2500

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
Bilala Muslim Mission of Tanzania
P.O.Box 20033
Dar es salaam.

Yaliyomo

Dibaji	5
Utangulizi	6
Muhimu wa Qur'an na Kuhifadhiwa kwake kutokana na mabadiliko	8
Kutokea kwa Ahadith za Kuzusha	14
Kukiri kwa baadhi ya wazushi wa Ahadith	18
Baadhi ya Ahadith juu ya Aya zilizotolewa	20
Msimamo wa Masunni	23
Msimamo wa Mashi'a	26
Ni kwanini Uislamu wa Kimarikani wazitumia Ahadith hizi	28

D I B A J I

Qur'an ni chimbuko la Uislamau na muujiza wa Ki-Ungu wa Mtume wa Uislamu. Ni kitabu ambacho hufanya muongozo haswa kwa Waislamu. Sehemu ya muhimu wake katika Uislamu inaweza kuonekana kutokana na muhimu uliopewa katika uhifadhi wake, katika kuihifadhi kwa moyo na katika hali ya maandishi na Mtume, na wafuasi wake katika karne kumi na nne zilizopita za historia ya Uislamu.

Hakuna dhehebu katika ulimwengu wa Uislamu huu wa hitilafu ambayo ina mashaka juu ya usahihi na ukamilifu wa Qur'an. Bahati mbaya katika miaka kumi na tano iliyopita, baadhi ya vikundi vilianza kusambaza vijitabu na nyaraka ambazo ndani yake wamewalaumu Waislamu Mashia kwa ukafiri kwa sababu, kwa dhana yao Mashia hawaamini ukamilifu uliiopo kwenye Qur'an iliyopo sasa.

Lawama hizi zina ukweli gain, wenye kulaumu ni kwa kiasi gain wenyewe wawe huru na "dhambi" hii, na hatimaye ni nani ananufaika kutokana na fitna hii, ndio somo la uchunguzi huu uliofanywa katika njia isiyo na chuki kabisa na Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi. Hii iliwasilishwa kwanza kama mada katika "Islamic Thought Conference" (Taasisi ya Fikira ya Kiislamu) mjini Tehran (Iran) Januari 1992. Ilichapishwa katika Jarida letu la Kingereza **The Light**, na kutafsiriwa katika Kiswahili na Sheikh Dhikiri U.M. Kiondo na kuchapishwa katika jarida letu la Kiswahili **Sauti ya Bilal** mwaka 1992.Sasa ni furaha ya Bilal Muslim Mission of Tanzania kuwasilisha kitabu hiki cha Kiswahili kwa wenye kutafuta ukweli.

Tunamuomba Allah (S.W.T) Akifanye kitabu hiki kuwa ni nuru na kifungua macho kwa Waislamu.

Wa Ma tawfiq ila bi-llah.

Bilal Muslim Mission of Tanzania
P.O.Box 20033,
Dar es salaam.

UTANGULIZI

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa rehema , Rahimu

Qur;ani ndio msingi mkuu wa Uislamu, na ndio mujiza wa kudumu wa Mtukufu Mtume wetu Muhammad (s.a.w.w).

Allah (s.w.t.) ameahidi kuwa Mlinzi wa Mhifadhi wa Qur'ani. Kwa sababu hiyo Qur'ani iliksanywa na kuwekwa kwenye hali ya kutabu tangu kwenye zama za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwenye *Hadith ya Thaqalayn* anaiita "kitabu"; na Bwana Umar bin Khattab (kwenye *Hadith ya Qirtas*) anaiita "kitabu."

Maadui wa Uislamu walitaka kujenga shaka kuhusiana na usahihi wake, hivyo wakajinufaisha kutokana na soko lililostawi la Ahadith za kuzushwa na taarifa za kubuniwa zisemazo kuwa Qur'ani ilikusanywa kwenye hali ya kitabu muda mrefu baada ya kuondoka Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), na kwamba kutokana na huu ukusanyaji wa baadaye, mamia ya aya zake zilipotea na vifungu na maneno mengi yalibadilishwa.

Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliiweka Qur'ani kuwa ndicho kipimo cha *Ahadith*, lakini Waislamu walianza kuipima Qur.ani kwa *Ahadith*. *Ahadith* nyingi za aina hii zilipata nafasi kwenye ukusanyaji

1. Soma: Qur'ani. 15:9

wa *Ahadith* wa Masunni na Mashia.

Kwa bahati njema, hakuna hata Madhihebu moja ya Kiislamu iliyotia shaka kuhusiana na usahihi wa Qur'ani. Madhehebu zote zilitambua kuwa, kama *Hadith* yoyote ile ya aina hii haiwezi kutafsirewa, ni lazima ikataliwe na kutupiliwa mbali.

Lakini baada ya kufaulu kwa Mapinduzi ya Kiislamu nchini Iran, na mwito wan chi hiyo wa kuwaitia Waislamu wote kwenye Umoja wa Kiislamu, Uislamu wa Kimarikani na vibaraka wao wa Kisaudia na Kikuwaiti wameanza kuzichapisha na kuzihubiri Ahadith hizi kutoka kwenye vitabu vya Kishia. Na kuwahukumu Mashia kuwa ni *Kuffar* (Makafiri) kwa sababu ya Ahadith hizo. Lengo lao laonekana kana kwamba ni kuudhihaki Ushia, kuidhoofisha Iran na kuisimamisha idiolojia ya Ki-Irani ya "Udugu wa Kiislamu" yenye kuwahamamisha vijana wa Kiislamu, ili kuziokoa milki zao.

Lakini, lengo lao hasa ni kuuvunjilia mbali msingi wa uislamu, kuunda modeli ya Waislamu wa Kimarikani watakaoonekana kana kwamba wana hisia za Uislamu na Qur'ani, kama tulivyoona huko Uturuki, Algeria, Misri, Morocco, Tunisia na kwenye sehemu nyinginezo.

Lakini Allah Ataikamilisha Nuru yake japo makafiri wakirihishwe na jambo hilo.

و آخر دعوانا أن الحمد لله رب العالمين

Dar es Salaam. **Sayyid Saeed Akhtar Rizvi,**
Januari 1992

MUHIMU WA QUR'ANI NA KUHIFADHIWA KWAKE KUTOKANA NA MABADILIKO

Qur'ani ndio Muujiza wa kudumu na uthibistisho ulio hai hadi hivi sasa, kwa ukweli wa Uislamu na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Iliushinda upinzani wa kutaka kuleta mfano wake, hata aya moja tu iliyo mfano wa ile aya yake isemayo; "kama wanadhani kuwa (hii Qur'ani) haitoki kwa Allah", maadaui walishindwa kuleta mfano wake, na wakajaribu kuizima Nuru ya Uislamu kwa kuanzisha vita baada ya vita, ambayo kwa bahati bado yaendelea kwenye nyanja mbali mbali za mapambazuko kwa kutumia sura mbalimbali za kujifichia.

Shabaha yao kuu ilikuwa nab ado ingali kwamba, Qur'ani ambayo maadui hao wamekuwa wakijaribu kuikashifu kwa njia hii au nyingineyo, kwa mfano:

(1) Walisema kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) amejifunza misingi hii ya ukweli ulio madhubuti kabisa kutoka kwa Wayahudi au Wakaristo.

(2) Walidai kuwa kwenye Qur'ani mna vifungu vinavyopingana.

(3) Walijitahidi kueneza kwamba Maadili ya Qur'ani hayana kabisa mafundisho bora zaidi ya kimaadili yaliyomo kwenye dini ya Kikristo.

Hakuna hata moja ya madai haya lililoweza kujitetea mbele ya macho ya mwanafikara huru: Waislamu waliyakanusha madai yote haya. Tunahitaji tu kuyasoma mazungumzo ya Amirul Muminiin

yote haya. Tunahitaji tu kuyasoma mazungumzo ya Amirul Muminiin Ali bin Abi Twalib (a.s.) na *Zindiq* mmoja, juu ya Qur'ani. Ili kuona jinsi Imamu atokanaye na Ahlul Bayt (a.s), ambao ndio Walinzi wa ukweli wa Qur'ani, kwa mujibu wa *Hadith ya Thaqalayn*, alivyoihama Qur'ani na kuuthibitisha ukweli wake, kiasi cha mtu kutokana na shaka yoyote ile tena.

Mazungumzo haya yameshabahia katika kuonyesha kwamba haikuwepo *Tahrif* kwenye Qur'ani. Neno *Tahrif* linaweza kutoa maana kadhaa. Maana tunayohusika nayo hapa ni mabadilisho au uondoaji wa maneno. Ni itikaji yetu kwamba hakuna mabadililisho, wala maongezeo wala uondoaji wa maneno kwenye Qur'ani:

«إنا نحن نزلنا الذكر وإنا له لحافظون».

Hakika Sisi ndio Tuliouteremsha huu Ukumbusho na hakika sisi ndio Mhifadhi wake. (Al-Hijr, 15:9).

(Hebu izingatie hii misisitizo mitatu ya kifungu cha (vijana)

الجملة الثانية na «إنّ» na لام التأكيد

Katika uitimiza ahadi hii, Qur'ani ilikusanywa katika hali ya kitabu tangu kwenye siku za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w) mwenyewe.

Kutoka kwenye pande zote mbili, ule wa nje (kutoka kwenye *Sunnah*) na ule wa ndani (kutoka kwenye Qur'ani yenyewe) umethibitika ushahidi madhubuti kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) aliacha kitabu mikononi mwa Waislamu.

Ama kwa upande wa Qur'ani ziko aya zisizopungua hamsini na mbili ambazo Qur'ani imeitwa "kitabu".

Hadith maarufu sana na iliyo *Mutawatir* (yaani iliohadithiwa

na watu wengi sana kiasi cha mtu kutokuwa na shaka yoyote juu ya usahihi wake) ya *Thaqalayn* ipatikkanayo kwenye vitabu vya *Ahadith* vya Kishia na Kisuni inathibitisha kuweko kwa "kitabu" hiki Qur'ani kwenye siku za mwishoni za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Hadithi hii inahadithiwa kwenye vitabu vingi pamoja na mabadiliko yasiyo muhimu katika maneno, lakini sehemu muhimu ni zile zile kila mahali. Ninainakili Hadithi hiyo kutoka kwenye *Sahihi ya Muslim* ambamo sahaba Bwana Zaid ibn Argam anaitaja Hotuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w) huko Ghadiir Khum. Bwana huyo anahadithia hivi:

«وإني تارك فيكم الثقلين أولهما كتاب الله
فيه الهدىٰ و النور فخذوا بكتاب الله و إستمسكوا به» - فحث على
كتاب الله و رغب فيه ثم قال: «و أهل بيتي. أذكركم الله في أهل بيتي
أذكركم الله في أهل بيتي أذكركم الله في أهل بيتي.»

"Na ninakuachieni miongoni mwenu Vitu viwili Vizito. Cha kwanza ni Kitabu cha Allah; ndani yake mna Mwongozo na Nuru;hivyo, kishikilieni barabara na jiambatanisheni nacho. (Baada ya hapo aliwasihi watu kuhusiana na hicho Kitabu cha Allah na akawafanya wakitamani sana; kasha akasema: "Na (kitu cha pili) ni *Ahlu'l-Bayt* wangu; ninakukumbusheni Allah kuhusiana na Ahlu'l-*Bayt wangu*, ninakukumbusheni Allah kuhusiana na *Ahlul'l-Bayt* wangu.

Ziko Ahadith nyingi ambazo ndani yake maneno «كتاب الله و سنتي» (kitabu cha Allah na Sunnan zangu yametumiwa. Lakini maneno "kitabu cha Allah" yamo kwenye Ahadith hizo pia.

---

2. Soma: **Sahih Muslim**, chapa ya Beirut, toleo la 2, la mwaka 1972, juzuu 4, uk. 1873
Hadithi hii imehadithiwa na zaidi ya Masahaba 20 wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Vile vile soma Musnad cha Imam Ahmad ibn Hanbal, Juzuu 3, uk 14,17,26 na 59; Juzuu 4, uk. 366 na 371; Juzuu 5, uk. 182 na 189. *Muhaddithiin wengi* wameihadithia Hadith hii kwenye vitabu vyao.

Hii hotuba ya *Ghadiir Khum* ilitolewa kiasi cha miezi miwili na nusu kabla ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia na wakati huo kilikuwepo kitabu cha Allah ambacho Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akikiacha miongoni mwa *Ummah* wake na ambacho *Ummah* huo uliusiwa kujiambatanisha nacho.

Kisha siku chache tu kabla ya kufariki dunia kwake, Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema:

هلم أكتب لكم كتاباً لا تضلون بعده فقال عمر: إن رسول الله قد غلب عليه الوجع و عندكم القرأن حسبنا كتاب الله.

"…;Njoni nikuandikieni maandiko (ambayo kwayo) hamtapotea baada yangu". Lakini Umar akasema: "Hakika Mjumbe wa Allah kazidiwa na maumivu na ninyi mnayo Qur'ani; kinatutosha kitabu cha Allah…"

Maneno haya yaonyesha kwamba kilikuwepo kitabu cha Allah mikononi mwa Waislamu kabla ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia.

Ni makosa kabisa kufikiria kwamba neon "kitabu" kwenye Qur'ani kwenye Hutuba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kwenye kauli ya Hadrat Umar bin Khattab lilitumika kwa maana ya vipande vya karatasi vilivyotawanyika huko, n.k. Ustadhul Fagaha as-Sayid al-Khoui amesema kweli pale, baada ya kuitaja rejea ya Qur'ani na ile Hadith ya Ghadiir Khum, aliposema: "-uko uthibitisho wa dhahiri kwamba, wakati huo Qur'ani ilikuwa tayari ishaandikwa na kukusanywa kwa sababu neon "Kitabu" halitumiki

---

3. Soma: Sahih Muslim, chapa ya Beirut, Toleo la 1, la mwaka 1375 Hijiriya (sawa na 1955 Masihiya)
Juzuu 1, uk. 1295.
Bwana Bukhari ameitoa Hadithi hii kwenye sehemu 4 amabazo ni Sahih Bukhari, chapa ya Cairo, ya 1958, Juzuu 1 uk. 39; Juzuu 6, uk. 11-12; Juzuu 7, uk. 155-156; Juzuu 9, uk. 137.

kwa ajili ya kile kilichokaririwa, wala halitumiki kwa vipande vya maandiko yaliyotawanyika huko na huko, kwenye vipande vya makaratasi, mifupa, ila linapotumika kimfano. Lakini si sahihi kuichukulia maana ya neno kuwa ni ya kimfano mpaka uwepo ushahidi kwenye maneno yanayotangulia na kulifuatia neno hilo. Neno "kitabu" laonyesha kuwepo kwa mkusanyiko wa maandishi hayo, wala si mtawanyiko wake, wala si kuwepo kwa mambo yaliyokaririwa akilini bila ya kuandikwa".

Tangu kwenye siku za mwanzoni kabisa, maadui wa Uislamu waliunda makri ambayo waliidhania kuwa ifafaa kabisa katika kuidhoofisha itikadi juu ya usahihi na kutokuwa na kifani kwa Qur'ani, ambayo ndio msingi wa Uislamu.

Waliitazama hali ya ulimwengu wa Kiislamu iliyokuwapo wakati ule na wakaona kuwa ktayari lilikwishakuwapo soko, tena lenye kustawi la *Ahadith* za kuzusha. Wakalitumia soko hili kwa faida yao kwa kadiri walivyoweza na wakaanzisha kazi ya ujumla ya kuzizusha *Ahadith* wakiyatupilia masingizio juu ya usahihi wa Qur'ani, kwa kuzusha kwamba yalikuwapo maongezo, mapunguzo, mabadilisho na hata kusema kuwa yako makosa kwenye Qur'ani iliyomo mikononi mwetu.

Fikara hii ilikuwa na hadi hivi sasa ingali kinyume kabisa na kile wakiaminicho Waislamu wote, Mashia na Masunni, juu ya Qur'ani.

---

4. Soma: Al-Bayanfi Tafsiri'l QQur'ani cha as_Sayyid al-Khoui, chapa ya Kuwait ya mwaka 11399 Hijiriya (sawa na 1979 Masihiya).Vile vile soma tafsiri (ya Kiingereza ya sura zake mbili, iitwayo: "The Collection and Preservationof Qur'ani", (iliyotafsiriwa na Mulla Asgharali M. M. Jaffar, katika mwaka 1407 Hijiriya, sawa na 1987 Masihiya iliyochapishwa London). {*Bilal Muslim Mission Ina furaha kubwa kuwaarifu kwamba hivi karibuni tutachapisha Tafsiri ya Kiingereza cha Al-Bayanfi Tafsr'l Qur'an iliyotafsiriwa na mwandishiwa KItabu hiki na kiongozi wetu Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizwi*}

Ash-Shaykh Abu Ja'afar as-Sadiq (aliyefariki kwenye mwaka 381 Hijiriya) ameandika hivi:

Ni itikadi yetu (sisi Mashia) kwamba Qur'ani ambayo Allah amemfunulia Mtume wake Muhammad, ni hii iliyoko baina ya majadala mawili (*daffalayn*). Na ndio ile iliyoko mikononi mwa watu, wala kiasi chake si zaidi ya hiyo."

Kisha anaendelea kusema:

"Na mwenye kudai kuwa tunasema kuwa kiasi chake ni zaidi ya hiki (tulichonacho) yu mwongo.

---

5. Soma: **Kitabul'I Itiqad" cha** ash-Shaykh Abu Ja'ffar Saduq, chapa ya Tehran ya mwaka 1370 Hijiriya, uk 63.

Vile vile soma tafsiri yake ya Kiingereza iitwayo **"The Shi'ite Creed"** (iliyotafsiriwa na A.AA. Faizi) na Oxford University press, Bombay.

Tangazo la namna hiyo hiyo limeolewa karibuni na kila Mujtahidiin mkuu wa Kishia, kwa mfano:

(a) Ash-Shaykh Al-Mufid (aliyeishi baina ya mwaka 338 hadi mwaka 413 Hijiriya) kwenye kitabu chake kiitwacho **Awa'ilu'l-Maqalat**. Uk.95.

(b) Ash-Sharif al-Murtadha, kwenye kitabu chake kiitwacho **"Bahrul'I Fawa'id"**, chapa yta Tehran ya mwaka 1314 Hijiriya, uk.69.

(c) Ash-Shaykh at-Tusi (aliyeishi baina ya mwaka 385 hadi mwaka 408 Hijiriya)kwenye kitabu chake kiitwacho "**Tafsir at-Tibyan**", chapa ya Najaf, ya mwaka 1376 Hijiriya, Juzuu 1, uk. 3.

(d) Ash-Shaykh at Tabrasi, (aliyefariki dunia mnamo mwaka 548 Hijiriya), kwenye kitabu chake kiitwacho **Tafsir Majmaa'ul bayan**, chapa ya Lebanon Juzuu 1, uk. 15.

Itikadi hii imeendelea miongoni mwa Mashia bila ya kuingiliwa hadi hivi leo. Mtu anaweza kuyataja tu majina ya as-Sayyid Muhsin al-Amin (aliyeishi baina ya mwaka 1284 hadi mwaka 1371 Hijiriya), as-Sayyid Sharafu'd-din (aliyeishi baina mwaka 1290 hadi mwaka 1377 Hijiriya), ash-Shaykh Muhammad Husayn Kashifu'l Ghita (aliyeishi baina ya mwaka 1295 hadi mwaka 1337 Hijiriya), as-Sayyid Muhsin al-Hakim (aliyeishi baina ya mwaka 1306 hadi mwaka 1390 Hijiriya), as-Sayyid al-Milani (aliyeishi baina ya mwaka 1313 hadi mwaka 1390 Hijiriya), al-Allamah at Tabatabai (aliyeishi

baina ya mwaka 1321 hadi mwaka 1402 Hijiriya), as-Sayyid al-Gulpaegani (Allah na Ambakishe hai) na as-Sayyid al-Khoui (Allah na Ambakishe hai). [As-Sayyid Gulpaegani (aliyeishi baina ya mwaka 1316 hadi mwaka 1414 Hijiriya) na as-Sayyid al Khoui (aliyeishi baina ya mwaka 1317 na mwaka 1413 Hijiriya]

ya hiki (tulichonacho) yu mwongo.

Ningalipenda nitoe maelezo machache juu ya mambo sita yafuatavo kuhusian na maudhui hii, ili nionyeshe jinsi maadui wa Uislamu walivyopata nafasi ya kujenga *Fitna*h au *Tahrif* na kisasi cha kufaulu kwao kwenye juhudi zao hizo.

1. Kutokea kwa Ahadith za kuzusha kwenye ulimwengu wa Kiislamu.
2. Kukiri kwa baadhi ya wale waliojitumbukiza kwenye kitendo hiki (cha kuzusha Ahadith).
3. Mifano ya hizo Ahadith za kuzushwa zionyeshayo kwamba mamia, kama si maelfu, ya aya za Qur'ani yaliyoondolewa kutoka kwenye Qur'ani.
4. Msimamo wa Masunni, na itikadi yao. Njia ya uondoaji wa Qur'ani na maana yake.
5. Maoni ya Mashia kuhusiana na Ahadith hizo.
6. Uislamu wa Kimarikani uliifufua maudhui hii iliyokwisha kuzikwa, kwa kuonyesha kana kwamba wanaushutumu Ushia na kuzizuia juhusi za Wairani za kuudumisha umoja wa Kiislamu duniani kote. Lakini shahada yake hasa ilikuwa ni vipi?

Ni dhahiri kwamba muda hauturuhusu kuyazungumzi mambo haya kwa undani zaidi. Hivyo basi, ninataka nizizungumzie maudhui hizi kwa muhtasari tu kwenye mazungumzo haya.

(A) KUTOKEA KWA AHADITHI ZA KUZUSHA:

Ni jambo lisikitishalo kuona kwamba watu wameanza kumhusisha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ahadithi za kuzusha hata kwenye zama za uhai wake. Ilimbidi Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuuonya *Ummah* kuhusu *fitnah* hii kwa maneno haya:

لقد كثر عليَّ الكذابة و ستكثر فمن كذَّب عليَّ متعمداً فليتبوأ مقعده من النار. فاذا أتاكم الحديث فأعرضوه على كتاب الله و سنتي فما وافق كتاب الله فخذوا به و ما خالف كتاب الله و سنتي فلا تأخذوا به.

"Hakika wako watu wengi waliozua uwongo dhidi yangu, na hakika idadi yao itaongezeka; yeyote yule anizulaye uwongo kwa kukusudia hana budi kujitayarisha makazi yake Motoni. Hivyo basi, kila mnapohadithiwa Hadith, itieni (kwenye kipimo) mbele ya Kitabu cha Allah na sunnah zangu (zilizodumishwa), na kila chenye kukubaliana na Kitabu cha Allah kichukueni; na kila kiendacho kinyume na kitabu cha Allah na Sunnah zangu, kikataeni".

Hadithi hii mashuhuri ni muhimu sana na ninakuomba uizingatie. Hatuna budi kutambua kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameiteua Qur'ani kuwa ndicho kipimo cha kuipimia *Hadith*, wala si kwamba Qur'ani ipimwe kwa *Ahadith.*

Amirul Mu'miniin Ali bin Abi Twalib (a.s.)aliulizwa ni kwa nini kuna tofauti kwenye Ahadith zilizohusishwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), yeye alipolijibu swali hili akasema:

"Kwa hakika mambo yazungumzwayo miongoni mwa watu, yako yaliyo sahihi na yako yasiyo sahihi, yaliyo kweli na yaliyo uwongo, yeye kuondoa kauli nyingine za kabla yake na yenye kuondolewa, ya ujumla na yenye kuwahusu watu maalum, ya dhahiri na yasiyo dhahiri, yaliyo hasa na yaliyo dhana. Hata kwenye zama za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) maneno ya uwongo

6 soma: Safinatul Bihar, cha Shaykh Abbas al Qummi, Juzuu 2, uk. 474. Vile vile Ahadith zisizo na idadi juu ya jambo hili zaweza kuonekana kwenye vitabu vya Madhehebu zote mbili (Shia na Sunni), ikiwa ni pamoja na Sahih Bukhari, Juzuu 1. uk 38.

yamehusishwa naye sana kiasi kwamba ilimbidi aseme kwenye hotuba yake, kwamba: “ye yote yule amzuliaye uwongoanajitayarisha makazi yake Motoni.” Wale wazihadithiano Ahadith wamegawanyika makundi manne, wala si zaidi ya hayo.”

Kisha akasema kwamba kundi la kwanza ni la wanafiki wasemao uwongo.

Mnafiki ni mtu ajionyeshe kuwa kasilimu na akajionyesha kuwa yu Mwislamu; hasiti kutenda dhambi wala hajiepushi na maovu; kwa kudhamiria kabisa humzulia uwongo Mjumbe wa Allah Amani na Barka za Allah na zimshukie yeye na Dhuria wake kama watu wangejua kwmaba yeye yu Mnafiki na mwongo, wasingekipokea kitu chochote kile kutoka kwake na wasingeyathibitisha maneno yake. Bali wanasema kuwa yu sahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), yeye kamwona Mtume (s.a.w.w.) ,amesikia (*Ahadith*) kutoka kwake, na akajipatia (elimu) kutokana naye. Hivyo wakayakubali yale ayasemayo. Allah naye amekuonyeni vizuri sana juu ya wanafiki na akakuelezeni juu yao kwa kirefu mno. Wanafiki waliendelea baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Hata hivyo, hali iliharibika zaidi baada ya kufariki dunia kishahidi kwa Saidina’ Ali (a.s), wakati *amir* Mu’awiyah alipokianzisha kile kiwezacho kuitwa idara ya kwanza ya Propaganda ulimwenguni. Hapa si mahali pa kutolea maelezo marefu zaidi juu ya jambo hili. Wale wanaopenda kujua zaidi na wasome *Sharh Nahjul,l-Balaghah*, ya Ibn Abi’l Hadi al-Mu’tazili ambaye amenukuu kwa maneno yenyewe hasa, kutoka kwenye kitabu kiitwacho *Kitabul-Ahadith* cha Abdul Hassan’Ali Ibn Muhammad Ibn Abi Sayf al-Mada’ini, maneno yaonyeshayo jinsi idara hii ilivyoendelea hatua hadi hatua, hadi Ahadith walizozizusha zilipojipenyeza kwenye ulimwengu mzima wa Kiislamu; watoto walifundishwa Ahadith hizi, kwenye Madrasah kama

---

7.Soma: Kitabu cha Hotuba za Saidina Ali (a.s) kitwacho Nahjul-Balaghah, tafsiri ya kiingereza iliyotafsiriwa Alai raza, na kuchapishwa na WOFIS (Tehran Iran), juzuu 2,uk. 453-454.

Walivyofundishwa Qur'ani. Anataja jinsi maradhi hayo yalivyovikumba vikundi vyote hasa wale walioonyesha uchamungu walisoma Qur'ani na wakafundishwa kuwa wachamungu. Walikuwa na desturi ya kuzusha Ahadith ili kutafuta kupendwa na watawala. Hatimaye *Ahadith* hizi ziliwafikia watu waliojawa na fikra za kidini hasa ambao hawakukubali kuwa kwenye *Ahadith* hizo mna uwongo na masingizio. Walizipokea Ahadith hizo kuwa ni sahihi kabisa na wakazihadithia kwa watu wakifikiria kuwa zilikuwa ni Ahadith sahihi za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Wahadithiaji wane wa Ahadith walikuwa kiini cha idara hii. Lakini yalikuwapo mamia ya askari waliopatikana kwa urahisi sana, ambao waliiuza dini yao kwa kujipatia faida za kidunia. Hapa chini tunalieleza tukio moja ili tu kuonyesha mfano wa hali hii.

Safari moja Amir Mu'awiyah alikuwa tayari kumpa sahaba mmoja aliyeitwa Samrah ibn. Jundab dirhamu laki moja (100,000) iwapo ataweza kutoa (kuzusha) Hadith ionyeshayo kuwa Aya 204 na 205 za *Sura al Baqarah* zilifunuliwa juu ya Ali Ibn Abi Twalib na kwamba aya 207 ilifunuliwa kwa kumsifu Abdur Rahman Ibn Muljim (mtu aliyempuga dharuba Saidina Ali (a.s) na kusababisha kifo chake).

Aya hizo ni hizi:-

"Na miongoni mw watu yuko yule ambaye kauli yake kuhusu maisha ya dunia hii inakustaajabisha (kwa kuyafurahia kwake), naye kumshuhudisha Allah yale yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye yu mpinzani mkubwa zaidi (ya wote). Na anapogeuka (kutoka kwako), anakimbia (huko na huko) katika nchi kufanya ufisadi humo, na kuangamiza mazao na mifugo na Allah hawapendi Wafisadi."

---

8. Soma: "Sharh Nahju'l-Balaghah" ua Ibn Abi'Hadid, kilichochapishwa na Daru Ihya'il Kutubil 'Arabiyah, Cairo, Juzuu 11, uk. 44-46.
9. Soma: "Sharh Nahju'l Balaghah" ya Ibn Abi'l Hadd, kilichochapishwa na Daru Ihy'il Kutubil ' Arabiyah, Cairo, juzuu 4, uk 63.

na aya ifuatayo ihusishwe na Ibn Muljim:

"Na miongoni mwa watu yuko aiuzaye nafsi yake kwa kutaka radhi ya Allah; na hakika Allah Yu Raufu kwa mja (wake mwaminifu)"

(Al-Baqarah, 2:207)

Hata hivyo, Bwana Samrah hakukubali. Kima kile kiliongezwa na kufanywa dirhamu laki mbili lakini kufanya hivyo hakukumsaidia Muawiyah. Mwishoni Muawiyah akampa dirhamu laki nne, na Samrah akakubali na akato (akazusha) Hadithi juu ya jambo hilo.

(B) KUKIRI KWA BAADHI YA WAZUSHI WA AHADITH:

kwa bahati mbaya kama tulivyuoeleza hapo juu, hata wale watu waliofikirriwa kuwa ni wema walijitumbukiza kwenye uzushi huu. Sahaba Bwana Abu Ismah aliulizwa hivi:

"Je umezipata wapi *Ahadith* zote hizi zilizopokewa kupitia kwa Ikrimah, kutoka kwa Ibn 'Abbas, kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), zenye kuelezea juu ya thawabu za kusoma kila Sura- ya Qur'ani Tukufu?" akajibu akisema: "Niliwaona watu wakipendelea Fighi ya Abu Hanifah na Maghazi ya Ibn Ishaq tu; hivyo basi nilizizusha *Ahadith* hizi kwa ajili ya kuitafuta radhi ya Allah" ili niwarudishe watu hawa kwenye Qur'ani".

Kilikuwepo kipindi amabcho uzushi wa *Ahadith* ulikuwa kawaida ya ulimwengu wa vyuo vya Kiislamu na makafiri, *Zanadiqah* na wanafiki walijinufaisha kutokana na kawaida hiyo

---

10. Soma: Sharh Nahju'l – Balaghah" ya Ibn Abi'l Hadid, kilichochapishwa na Daru Ihya'il Kutubil ' Arabiyah, Cairo, Juzuu 4, uk 63.
11. Soma: Fajru'l Islam, cha Bwana Ahmad Amin, chapa ya Misri, uk 215.

kwa kadiri walivyoweza. Walizusha maelfu ya *Ahadith* zote hizo zokihusishwa na kupokea kupitia kwa Masahaba maarufu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ili kuiharibu kazi ya Uislamu, kuudhoofisha msingi wake na kuliangusha jingo lote. Kwa mfano kafiri maarufu aitwaye Abdul Karim Ibn Abi'l Awjah alijukumiwa kifo na Gavana wa Kufah, alipokaribia kungongwa alisema: "Vema! Hata kama mninyonge nimekwisha kuzusha Ahadith elfu nene zenye kuiharmaisha *halal*i na kuihalalisha *haram*. Ninaapa kwa jina la Allah kwamba nimkwisha kukufunguzeni kwenye siku ya kufunga na kukufungisheni kwenye siku ya Idd.

Lakini makri hii isingeweza kufaulu ila pale Waislamu watakapofanywa waamini kuwa Qur'ani hakukusanywa kwenye zama za uhai wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), bali iliksanywa baadae kidogo kidogo kutoka makaratasini, vigaeni na mifupani kiasi cha miaka ishirini na mitatu baada ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kufariki dunia.

Waliifahamu vizuri sana saikolojia ya vikundi mbalimbali vya Waislamu wakaanza kuwapeleka fikara zipingazo Uislamu zilizofichwa kwenye *Fadhilat za Sahabah* au za Maimamu wa *Ahlu'l Bayt* ili kuwapotosha Masunni na Mashia, watu walinyweshwa sumu hii kwa kutiliwa kwenye sharubati na bila ya kusita, watu wakaimeza.

Cheo cha kuikushanya Qur'ani alikipewa Hadhrat Abu Bakr au hadharat uthman. Kila mzushi alizitumia dhana zake mwenyewwe na jambo hili llikazaa idadi kubwa ya *Ahadith* zenye kupingana.

As-Sayyid Al-Khoui amezizungumzia kwa makini Ahadith zote zihusuzo siku za baadaye za ukusanyaji wa Qur'ani na hatimaye akaamua kuwa Khalifa wa tatu (Hadhrat uthman bin Affan)

---

12. Soma: Vitabu hivi, Tarikh ya at tabari, Juzuu 8 uk 48, kilichochapishwa na Daru'l Mazinif: Tarikh al-Kamil ya Ibunu'l-Athir, juzuu 4, uk 7.

hakuikusanya Qur'ani. Alichokifanya ni kuwakusanyia Waislamu kwenye usomaji ambao ulifuatwa mjini Madina na akakataza aina nyinginezo za usomaji wa Qur'ani, zilizoibuka hapa na pale . Wanaopenda kujifunza zaidi juu ya jambo hili, na wasome kitabu chake kiitwacho al-Bayan kuanzia Uk. 187 hadi Uk. 278.

Hata hivyo ilipokwisha kudumishwa hii Hadithi ya ukusanyaji wa baadae wa Qur'ani Tukufu, ilikuwa rahisi kueneza *ahadith* zionyeshazo kwamba aya nyingi, hata baadhi ya Sura zilipotea na hazikuweza kupatikana wakati Hadhrat Abu Bakr na/au Hadhrat Uthman alipotaka kuikusanya Qur'ani katika hali ya Kitabu. Walivihusisha vifungu hivyo vya maneno na Mashaba wakuu na wakeze Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).

Wakitiwa usingizi na *Ahadith* hizi,Waislamu walisahau kabisa kwamba, Allah Mwenyewe Yu Mlinzi wa Kitabu Chake nakwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ameteua Qur'ani kuwa kipimo cha kupimia usahihi wa *Ahadith*. Waliipindua meza na wakaanza kuupima usahihi wa Qur'ani kupitia *Ahadith* hizo za kuzusha.

© BAADHI YA AHADITH JUU YA AYA ZILIZOTOLEWA

Haiwezekani kutoa maelezo kamili juu ya zote, sentesi zote na vifungu vyote vinavyodaiwa kuwa vilipotea wakati Qur'ani ilipokuwa ikikusanywa. Mifano michache yenye kung'ara inatolewa hapa chini kama ifuatavyo:-

(1) Sura ya 33 – al-Ahzab inadaiwa kwamba ilikuwa na aya 200 au karibuni Aya 300, amazo zote zimepotea ila zile Aya 73 tu tulizo nao hivi sasa.

Dai la Aya 200 linahusishwa na Ummul Muuminiin A'ishah ambaye anadaiwa kuwa alisema:-

و أخرج أبوعبيد في الفضائل و ابن الأنباري و ابن مردويه عن عائشة قالت: كانت سورة الأحزاب تقرأ في زمن النبي مائتي آية فلما كتب عثمان المصاحف لم يقدر منها إلا علىٰ ما هو الآن.

"Imehadithiwa na Abu "Ubayd kwenye kitabu chake kiitwacho al-fadha'il na Ibn *al-Anbari* na Ibn Maduwayh, kutoka kwa A'ishah kwamba Bibi huyo alisema:, Sura *Al-Ahzaab* ilikuwa ikisomwa kwenye zama za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa aya mia mbili, lakini Uthman alipoiandika Qur'ani alishindwa kupata zaidi ya kile tulichonacho hivi sasa.

Hivi sasa kuna Aya 73 tu kwenye Sura hii.

Inasemekana kwamba mtu mmoja aliyeitwa Hudhayfah alidai kuwa Aya 70 zilipotea.

Lakini Ubbay ibn Ka'b alifanywa aseme kuwa sura hii ilikuwa sawa au hata kuwa ndefu kuliko sura ya *al-Baqarah.* Vuile vile Tabi'I Ikrimah amehadithiwa kuwa alisema hivyo hivyo.

Sura ya *Al-Baqarah* ina Aya 286. Hivyo basi, ina maana kwamba aya 213 au zaidi zilipotea, ikiwa ni pamoja na Aya ya Kurujumu (kupiga mawe wazinifu hadi wafe).

(2) Sura ya tisa ya *At-Tawabah*: Inadaiwa kwamba theluthI mbili au robo tatu ya Sura hii imepotea. Taarifa hii inahusishwa na

13. Kwa maelezo zaidi soma vitabu hivi: **ad-Durru'l-Manthur**, cha as-Suyuti, Juzuu 5, uk. 179-180; **al-Itqan**, cha Suyuti, juzuu 2, uk 25.
14. Soma kitabu kiitwacho **at-Tarikh**, cha al-Bukhari, kama kilivyonukuliwa kwenye vitabu viwili tulivyovitaja kwenye Na. 13 hapo juu.
15. Soma vitabu hivi: Tafsir **al-Kashshaf** cha az-Zamakhshari, Chapa ya Misri, Juzuu 3, uk. 248; **Kanzu'l Ummal** cha Mulla Ali Muttaqi.
16. Soma vitabu hivi: **ad-Durru'l Manthur**, cha as-Suyuti, Juzuu 5 uk. 179.
17. **ad-Durru'l Manthur** cha as-Sayuti, juzuu 3 uk 208; **al-Itaqan** cha Suyuti, Juzuu 2 uk. 26; **all-Mustadrak**, cha al-hakim an-Nishapuri, chapa ya Haydarabad (India), Juzuu2, uk. 331.
18. Soma**: al-Itqan**, cha al-suyut, Juzuu 1 uk. 65.

Hudhayfah al-Yamani Imamu Malik ibn Anas aliulizwa ni kwa nini hakuna “Bismillah….” Kwenye sura hii. Imamu Malik akajibu: “ Ilipotea pamoja na sehemu yake ya mwanzoni kwa sababu inathibitishwa kwamba, sura hii ilikuwa sawa na sura “*al-Baqarah* kwa urefu”.

Lakini hivi sasa kuna Aya 127 kwenye sura hii, kwenye Qur’ani.

Ninadhani kuwa hakuna haja ya kuzitaja surah dhaifu za al-Khal” na al-Hafd, na surah nyingineyo iliyo sawa na Surah ya al-Bara’ah, ambazo zasemekana kwamba zimepotea kabisa; sura mbili za kwanza (al-Khl’ na al-Hafd) zasemekena kwamba zimeandikwa na Ubayy ibn Ka’b kwenye Qur’ani na Abu Musa al-Ash’ari, na ile sura ya tatu inasemwa na Abu Musa al-Ash’ari.

Muda hautoshi kuonyesha upuuzi wa sentesi kwenye sura hiyo zidaiwazo kuwa za *al-Khal’* na *al-Hafd.* Baadhi ya makosa ya kisarafu kwenye sentensi hizi yaonyesha wazi wazi kwamba mtu aliyezizusha sura hizi hakuwa na ujuzi wa kutosha wa lugha ya kiarabu. Na hizo sentensi zisizo sahihi zimehusishwa na masahaba kama vile Hadrat Umar, Ubay ibn Ka’b na Abu Mussa al-Ashari!

Kwa bahati mbaya Ahadith zenye kuondosha kukubwa au kudogo zimehusishwa na watu wakubwa katika Dini ya Kiislamu, kama vile Abdallah ibn Abbas, Abdallah ibn Mas’ud, Abdur Rahman ibn ‘ Awf, Zaid ibn Argam, Jabir ibn Abdallah, Buraydah, Maslamah ibn Makhlad, Abu Waqid al-Laythi, Ummul-MuuminiinHafsah, Ummul-Muminiin Ummu Salimah, na shangazi yake Abu Amamah ibn Sahl, na zaidi ya hapo zinahusishwa na Tabi’I Ikramah. Hadithi hizi zipatikana kwenye *sahih al Bukhari, sahih Muslim,*

---

19. Soma kitabu hicho al-Itqan.

20. Soma: Jami’u’l Usul, cha Ibnu’l Athir, chapa ya Misri, ya mwaka 1370 Hijiriya, Juzuu 3 uk. 8 Hadith Na. 904

21. Soma: Itmam-e-Hujjat, cha Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi, kilichochapishwa Faizabad (India), mwaka 1986, uk. 33-72.

Sunnan Abi Dauudi, Sahih Tirmidhi, Susan Nasai, Sunan Bayhaqi, *Musnad* ya Imam Ahmad ibn Hanbali, Muwatta ya Imam Malik, Tarikh ya al-Bakhari, Fathul Bari (ambacho ni sherehe ya Sahih Bukhari) cha Ibn Hajar al-Asqalani, Tafsir ad-Durru'l Manthir na al-Itgan (ambayo vyote viwili vimeandikwa na as-Suyuti)

Vile vile Ahadith zilihusishwa na Maimamu wa Ahlul Bayt (a.s) pia na zikapata njia ya kuviingiza vitabu vya Kishia vya Ahadith. Kwa kifupi ni kwamba, vitabu vya Ahadith vya Kisumi na Kishi'a vinazo *Ahadith* nyingi za aina hiyo. Lakini iko tofauti kubwa baina ya hizi madhehebu mbili kuhusiana na msimamo wao juu ya *Ahadith* hizi.

(D) MSIMAMO WA MASUNNI

Msimamo wa ndugu zetu hawa kuhusu *Ahadith* hizi umeathiriwa na itikadi yao ya kwamba *Ahadith* za Sahih Sittah (yaani vile vitabu sita vya *Ahadith* vichukuliwavyo kuwa ni sahihi), na hasa zile Ahadith zilizomo kwenye *Sahih al Bukhari* na *Sahih Muslim* zote ni sahihi kabisa.

«و تلقي الأمة بالقبول إنما أفادنا وجوب العمل بما فيهما و هذا متفق عليه - فإن أخبار الآحاد التي هي في غيرهما يجب العمل بها اذا صحت اسانيدها و لا تفيد إلا الظن وكذا الصحيحان - و انما يفترق الصحيحان و غيرهما في كون ما فيهما صحيحا لا يحتاج الى النظر فيه بل يجب العمل به مطلقاً - و ماكان في غيرهما لا يعمل به حتىٰ ينظر و يوجد فيه شروط الصحيح.»

(Ukweli uliopo kwamba *Ummah* umezikubali bila ya kusita hizi Sahih mbili – za al-Bukhari na Muslim) umetufanya tutambue kuwa ni wajibu kuyatekeleza yale yaliyoandikwa kwenye vitabu hivi viwili, na imekubaliwa hivyo kwa pamoja. Watu wanawajibika kuitekeleza *Khabar-ul-Wahid* iliyomo kwenye vitabu vinginevyo

iwapo nyororo ya wahadithiaji wake ni sahihi, na hata hivyo) haitadumisha chochote ila dhana yenye nguvu. Hali kadhalika kwa hizi Sahih mbili; lakini Sahihi hizi zatofautiana na vile vitabu vingine kwa sababu yote yapatikanayo kwenye hizi sahih mbili huchukuliwa kuwa ni sahihi na kwamba hakuna haja ya kuyachunguza; na badala yake ni *Wajib* kuyafuata bila ya sharti lo lote, lakini kuhusu zile *Ahadith* zilizomo kwenye vitabu vinginevyo hazitafuatwa mpaka thibitisho zake zichunguzwe na zithibitishe kuwa zinayatimiza masharti ya usahihi wa *Ahadith*.

Hili blangeti lisilo na masharti yo yote yale la kuzikubali *Ahadith* zilizomo kwenye vitabu hivi limewalazimisha ndugu zetu hawa kuikubali njia ya نسخ التلاوة usomaji wa kuondoa; hii ina maana kwamba wao huamini kwamba, usomaji wa baadhi ya Aya uliondolewa ingawa sheria iliyoendelezwa kwenye baadhi ya Aya hizo iliendelea. Mifano miwili iliyo maarufu mno ya Aya hizo zenye kudaiwa ni zile Aya ziitwazo Aya الرجم za (kurujumu) na Aya ya manyonyesho kumi au matano, zilizomo kwenye *Sahih al Bukhari* na *Sahih Muslim* na vitabu vinginevyo. Na Hadith iliyomo kwenye Sahih Muslim yasema wazi hivi:-

عن عائشة أنها قالت:

كان فيما أُنزل من القرآن عشر رضعات يحرّمن ثم نسخن بخمس رضعات - فتوفي رسول الله ﷺ و هن فيما يُقرأ من القرآن.

---

22. Soma: "Sharh Sahih Muslim", cha An-Nawawi,
23. Kuhusu Aya za Kurujumu, tafadhali tazama: Sahih al-Bukhari, Juzuu 4, uk. 179, 265; Sahih Muslim, Juzuu 3, uk 1317; Musnad, cha Ahamad ibn Hanbal, chapa ya Misri, Juzuu 1 uk. 40; Sunan, cha Ibn Majah, chapa ya kuhusu Aya za Unyonyeshaji, tafadhali soma: Sahihi Muslim, Juzuu 4, uk 167; ad-Durru'l Manthur, cha Suyuti, Juzuu 2, uk 135.

Ummul Muuminiin ‘ Aisha alisema: “Miongoni mwa yale yaliyofunuliwa kwenye Qur’ani ilikuweko (Aya): “Maonyesho kumi yafahamikayo hufanya maharamisho” (yaani hufanya ndugu wa kunyonyesha). Baadaye Aya hiyo iliondoshwa kwa Aya yenye “maonyesho matano”, na Mujumbe wa Allah alifariki dunia na hali manyonyesho hayo yakiwa miongoni mwa maandiko ya Qur’ani yaliyokuwa yakisomwa”.

Hapa swali huibuka: “Ni nani mwenye haki ya kuiondoka Aya ya qur’ani baada ya kufariki dunia kwake Mtukufu mtume (s.a.w.w.)? ndio sababu as-Sayyid al-Koui amesema:

و غير خفي أن القول بنسخ التلاوة هو بعينه القول بالتحريف و الإسقاط.[1]

“Nani ni dhahiri kwamba” njia ya uondoshaji wa usomaji “ ni sawa kabisa na itikadi ya mabadiliko na uondoaji kutoka kwenye Qur’ani.”

Hivyo basi, inatubidi kujiambatanisha na msingi uliodumishwa bara bara kwamba, Ahadith yoyote ile iendayo kinyume na Qur’ani ni lazima ikataliwe na “itupiliwe mbali kwenye ukuta”. Kama haiwezi kutafsiriwa kwa njia inayokubalika.

---

24. Soma: Sahih Muslim, Juzuu 4, uk 167; ad-Durru’l Manthur, cha Suyuti,Juzuu 2, uk. 135.
Baadhi ya vitabu vinamwelezea mama huyu kuwa kulikuwa na karatasi iliyokuwa na amri ya kuwarujumu na kuwanyonyesha watu wazima, chini ya mto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Alipofariki dunia, na watu walipokuwa wakijishughulisha na maziko yake, mbuzi aliingia nyumbani humo na akalila karatasi hilo. Hivyo karatasi hilo likapotea kabisa. Taarifa hizi tunazikuta kwenye: Musnad cha Ahmad ibn Hanbal, chapa ya Misri ya mwaka 1313, Hijiriya, Juzuu 6, uk. 269; Sunan Ibn Majah ul. 626; Tawii lu Mukhtalifl-hadith (cha Ibn Qutayban), chapa ya Misri, uk. 210.

25. Soma: Al-Bayan fi Tafsir’l Qur’an cha Imam al-Khoui, uk. 224.

(E) MSIMAMO WA MASHI'A

Iko mikusanyo mine ya awali zaidi ya *Ahadith* za Kishi'a ambayo kwa pamoja inaitwa "Vitabu Vinne vya Awali" – *al-Kafi, Man la Yahdhurhu'l Faqih, Tahdhibu'l ahkam na al-Istibsar.* Ingawa vitabu hivi vinashimiwa sana, katu Mashi'a hawajaviita Sahih. Hivyo basi, wao hawafungwi na Hadith yoyote iliyoandikwa kwenye chochote kati ya vitabu hivyo kwa sababu to imo kwenye kimoja kati ya vitabu hivyo. Badala yake wanazitia *Ahadith* za vitabu vyote hivi kwenye uchunguzi mkali , kuhusiana na asnad (wanadithiaji) zao, na *dirayah*, na kuchunguza kama kila Hadith inaafikiana na Qur'ani kauli zikubalikazo za Ma'sumiin na kweli zilizo maarufu. Kama Hadith ikipasi mtihani huu mgumu, basi itakubalika. Kama ikishindwa, basi hufasiriwa kwa njia ikubalikayo, na kama ikishindwa hapo hapo, itkataliwa moja kwa moja.

Hapa hatuna budi kusema kuwa, sehemu kubwa ya Ahadith zizungumziazo juu ya Tahrif ni zenye dosari na dhaifu kwa kadiri nyororo za wahadithiaji wao zihusikavyo. Hata hivyo, baadhi ya Ahadith hizo zaweza kuchukuliwa kuwa na maana ya kwamba, kulitokea ufasiri mbaya kwenye baadhi ya Aya, na kuzipa maana isiyo sahihi,. Fungu jingine la Ahadith laweza kuchukuliwa kwa urahisi kuwa linaieleza tafsiri ya pambizoni ya wahadithiaji wao.

Lakini bado zinasalia Ahadith nyingi zisizoweza kuelezeka kwa njia yoyote ile kati ya njia hizo mbili; na wanavyouoni wetu bila ya kusita wamezikataa kwa sababu zinakwenda kinyume na Qur'ani na Sunnah na ziko kinyume na Ijmah ya Ummah kwamba katu hayakuwepo maongezo au mapunguzo kwenye Qur'ani.

Mwanachuoni mmoja, Muhaqqiq al-Kalbasi amesema: "Taarifa zote hizi zizungumziazo juu ya Tahrif ziko kinyume na Ijma'h na hivyo basi si zenye kutengemewa ila kwa idadi ndogo sana ya watu.

---

26. Soma Al-Bayan fi Tafsir'l Qur'an cha Imam al-Khoui, uk. 253.

Mwandishi wa Sharh wa kitabu kiitwacho *al-Wafiyah, Muhaqqiq al-Baghdadi* amesema wazi wazi, kwa kunakili vifungu kutoka kwenye kitabu cha *Muhaqqiq al-Karkai* (aliyeandika kitabu kamili juu ya Maudhui hii), amesema kwamba: “Ahadith zizungumziazo juu ya mpunguzo ni lazima zitafsiriwe upya au zikataliwe kabisa. Hadithi yo yote ile ipinganayo na Qur’ani, Sunaah zilizokwisha kuthibitishwa na Ijma’ ni lazima zikataliwe kama hazina nafasi katika kutafsiriwa upya au ufafanuzi ukubalikao”.

Hapa tunainukuu Hadith iliyoandikwa kwenye *al-Kafi* ili kutoa mfano kivitendo wa kile tunachokikusudia pale tunapozungumzia juu ya kuitafsiri upya hadith au kuitolea ufafanuzi uthibitisho usahihi wa hadith:-

عن أبي عبدالله عليه السلام قال: إن
القرآن الذي جاء به جبرئيل عليه السلام الى محمد صلى الله عليه وآله سبعة عشر ألف آية.

Abu’ Abdallah (Amani ya Allah na imshukie amesema: “Qur’ani aliyoileta Jibrili (Amani ya Allah na imshukie) kwa Muhammad (Amani ya Allah na imshukie yeye na dhuria wake) ni Aya elfu kumi na saba”.

Ash-Shaykh as-Saduq)r.a) ameandikwa kwenye kitabu chake kiitwacho Kitabu’l I’tiqaadat maneno ambayo, kwa maoni yangu ni sawa na kuitafsiri upya Hadith hii. Shaykh huyu anaandika hivi:-

Tunasema kwamba umeteremka ufunuo mweingi sana ambao

---

27. Soma: Al-Bayan fi Tafsir’l Qur’an.

28. Soma: Al-Kafi (كتاب فضل القرآن. باب النوادر) chapa ya Tehran ya mwaka 1388 Hijiriya, Juzuu 2 uk. 463.

"Tunasema kwamba umeteremka ufunuo mewing sana ambao si sehemu ya Qur'ani, kiasi kwamba kama ungalikusanywa bila shaka kiasi chake kingalikuwa aya 17,000. Na hii, kwa mfano, ni kama ile kauli ya Jibrili kwa Mtukufu Mtume," Allah anakwambia, Ewe Muhammad, kuwa mpole kwa viumbe vyangu, kama vile ni fanyavyo (mimi mwenyewe)."

Ash-Shaykh as-Shaykh as-Saduq (r.a) anaendelea kuzinukuu Ahadith qudsiyah hadi anamalizia kwa kusema:

"Ziko Ahadith qudsiyah nyingi za aina hiyo ambayo zote ni ufunuo, lakini si sehemu ya Qur'ani na mabazo kama zingelikuwa (sehemu ya Qur'ani bila shaka zinagalitiwa kwenye Qur'ani, na zisingeltengwa nayo"

Kama mtu hayuko tayari kuyakubali maelezo haya, kwa sababu Ahadith hizi zazungumzia kuhusu "Qur'ani basi tutaikataa hadith bila ya kusita. Sababu yake: Ingawa idadi (17,000) iliyotajwa kwenye hadith hii ni ndogo sana kuliko ile iliyotajwa na Khalifa wa pili (ya herufi milioni moja na elfu ishirini na saba kwenye Qur'ani), hata hivyo, idadi hii ni kubwa mara tatu kuliko idadi halisi ya Aya (ambazo hivi sasa ni aya moja moja elfu sita na mia mbili).

(F) NI KWA NINI UISLAMU WA KIMARIKANI WAZITUMIA AHADITH HIZI?

Kama tulivyoeleza hapo juu, maadui wa Uislamu wamefaulu kuzieneza Ahadith hizi zilizo kinyume na Qur'ani kwenye Ulimwengu wa kiislamu, wakizihusisha na watu wakuu katika Dini ya Kiislamu, huku Mashaba wa mtukufu Mtume (s.a.w.w) pamoja na Ahlul

---

29. Soma: Kitabu'l I'tiqad, cha Shaykh as-Saduq.
30. Soma: Al-Itqan, cha Suyuti, Juzuu 2 uk. 70.
    Lakini kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa, ziko herufi mia mbili-sitini na saba elfu na hamsini na tatu (267,053) kwenye Qur'an.

31. Wale wasiochukua jukumu la kuhesabu. Wanaendelea kuandika kuwa ziko Aya 6,666 kwenye Qur'ani . Huu ni mfano mwingine wa uzembe wa Waislamu wenye kuhuzunisha kuhusiana na Qur'ani.

Bayt wake (a.s); na pole pole Waislamu, bila ya kujua walizikubali na wakaziandika Ahadith hizi zilizo dhaifu na zakuzushwa kwenye mikusanyo yao ya *Ahadith.* Ijapokuwa ilitokea hivyo, 'ulama wa Kiislam, Wakishia na wa Kisunni, hawakuamini kuwa yalikuwapo maongezo au mapunguzo kutoka kwenye Qur'ani. Hakuna '*Alim* mwenye akili timamu kutoka kwenye madhehebu yo yote ile kati ya hizo aliyeishutumu ile madhehebu ya pili kuwa inaamini *Tahrif* ya Qur'ani. Ni kweli kwamba kwenye nyakati Fulani Fulani baadhi ya '*Ulama* kutoka kwenye pande zote mbili walijitia kwenye uipaka matope madhehebu ya pili, bila ya kutambua kuwa kuwepo kwa Hadith kwenye kitabu, si lazima kuwe na maana kwamba watu wa kundi hilo wanaiamini Hadith hiyo. Lakini Ahadith hizi zilizikwa vitabuni humo na hazikuhubiriwa kwa sababu tu kwamba hakuna mtu ye yote yule aliyeitengemeza itikadi yake kwenye *Ahadith* hizi.

Badiliko hili la ghafla kwenye mwezi wa Februari 1979, wakati taifa la Kirani, chini ya uongozi usio na kifani wa Marehemu Imamu al-Khomeini (rehema za Alla na zimshukie) lilifaulu kuisimamisha serikali ya Kiislamu ya kwanza ya kweli hapa duniani baada ya kupita karne nyingi tangu zama za Maimamu (a.s).

Kama mapinduzi ya Kiran yangezaa sreikali ya vibaraka, na ikafuata njia ya idiolojia ya Kimagharibi au ya Kimashariki, ingelipokea kwa furaha kuu – au japo kuvumiliwa tu na wale walinzi wa "Demokrasia" wakujiteua wenyewe. Lakini kinyume na hekima hiyo kawaida, ilichagua kuifuata njia ya Uislamu. Baada ya hapo ikaanza kuiinua hamasa ya udugu wa Kiislamu". Kwa kusimama dhidi ya mambo yote yasiyo ya Kiislamu, na kkutomsujudia yeyote yule ila Allah, Imamu Khomeini na uongozi wa Iran alipata umaarufu usio kifani kwenye Ummah wa Kiislamu, kila mahali ulimwenguni, tangu Morocco hadi Ufilipino, na kutoka Ulaya hadi Umarikani. Ummah uliokandamizwa ulijionea kwa macho yao kwamba mtu asiye na silaha, aliye mikono mitupu ameshinda

kwenye vita vya mashine za kivita kubwa zaidi huko mashariki ya kati. Mapinduzi haya yaliwapa watu wakandamizwao moyo mpya,

hata kwenye nchi zisizo za Kiislamu – kama vile Africa ya Kusini. Huu mvuto ulioenea haraka zaidi wa fikra za Ayatullah Khomeini uliithadharisha U.S.A., "chifu mkuu" wa "wakabila" ya Kimagharibi. Wakaanza kuipiga vita Iran, kwa kutumia vita vya mawakili kupitia vyombo vya habari katika mstari wa mbele mmoja,na katika mstari wa mbele mwingine wakawafanya mawakili wao huko Saudi Arabia na Kuwait waamini kwamba wito wa udugu wa Kiislamu hatari kubwa kwa viti vyao vya enzi. Mawahhabiyah wakiamriwa na mabwana zao, walianzisha propaganda iliyojaa chuki iliyo kali mno, dhidi ya "Fikara za Khomeini", Iran na Ushia. Kalamu zilizokodiwa zilianza kuvishkasuka vitabu, makala na vijitabu dhidi ya Mashia wakisema kuwa Mashia ni Kafir, ni Mushriki, wana Qur'ani yao na wanaamini kuwa hii Qur'ani waliyonayo Waislamu imebadilishwa na si kamili. Baadhi ya wafanyakazi wao wakuu zaidi ni Ihsan Ilahi Zahiir na Balighuddin wa Pakistan na manzuur Ahmad No'mani na abu Hassan Ali Nadwi wa India.

Mtu wa mwisho kutajwa hapo juu anashangaza mno. Siku nyingi kabla ya Mapinduzi ya Iran alijitokeza akiwa yu shujaa wa Umoja wa Kiislamu zimhusuzo mtu binafsi, nchini India, ambayo Makamu wa mwenyekiti wake n Alim wa Kishi'a. Lakini vile vile anapokea "Zawadi ya Faisal" ya ukoo wa bani Saudi. Na mara tu baada ya kutolewa hamasa ya "Si Mashariki wala Magharibi, Uislamu ndio bora zaidi, "ilipoanza kupelekwa kila mahali kutoka Iran, alijiunga pamoja na nguvu zipingazo Umoja wa Kiislamu. Kwenye kimoja kati ;ya vijitabu vyake alivyoviandika dhidi ya Ushia ameandika kuwa Mashia hawaiamini Qur'ani, ndio maana hakuna Hafidh-i-Qur'ni miongoni mwa Mashia. Mtu huyu aliendelea kuandika kuwa, safari moja alipoalikwa kwenda Iran, kundi la waalikwa lilipelekwa Qum ambako walimtembelea Ayatullah Mkuu. Shughuli za huko nyumbani kwa Ayatullah huyo

zilipangwa kuanzia na kisomo cha Qur'ani Tukufu, na mwana wa Ayatullah huyo, ambaye yeye mwenyewwwe yu Aalim, alisimama,

akafungua Qur'ani na akasoma aya Fulani Fulani kutoka kwenye hiyo Qur'ani. Kisha anasema: " Kwa upande wa itikadi yetu ya Kissuni, hata motto mdogo huikariri sura ndogo moja au mbili, lakini huyu Alim wa Kishia hakuweza kukukumbuka japo kiasi hicho tu. Hii ni kwa sababu Mashia hawaiamini Qur'ani.

Je, yuko mmoja wetu ategeaye kuisikia hoja ya kitoto kama hii kutoka kwa mtu huyu maarufu? Lakini yaonekana kana kwamba sauti itokayo kinywani mwake ni "Sauti ;ya Bwana wake" na jambia la Wasayuni lililochovywa kwenye damu ya waislamu linatumika katika sura ya kalamu yake.

Kitabu kinachoandikwa na vibaraka hawa chaweza kutokea kwa lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Kiarabu, urdu au lugha yo yote ile; lakini kwenye kipindi kifupi tu kitakuwa kimetafsiriwa kwa lugha zote zilizo kuu kwenye ulimwengu wa Kiislam, kukutawanya kila mahali na vile vile kikagawanyiwa Hujjaj (Mahujaji) bila ya kuwatoza malipo yoy oyote yale.

Kimatazamo, yaonekana kana kwamba hawa vibaraka wa Uislamu wa Kimarikani wanafanya hivi ili kuidhoofisha Iran na kuyazuia Mapinduzi ya Iirani yasiwaathiri Vijana wa kiislamu"- kama alivyokubali yeye mwenyewe Abul Hassn ' Ali Nadwi kwenye utangulizi wa kitabu Fulani. Lakini, je kufanya hivyo ndilo lengo la kuitamaduni la mabwana zao – Wakristo wa Kiyuda? "Hapana", si hivyo hata kidogo. Mwundo wa Uislamu wa Kimarikani umezichimbua baadhi ya hadith za Tahriif zilizozikwa vitabuni kwa sababu tu ya kwamba Mashia hawakuweza kulipiza kisasi kwa kuzitangaza Hadith zilizo kama hizo zipatikanazo kwenye vitabu vya Kisunni, na matokeo yake yakawa kwambaule usahihi wa Qur'ani ukaweza kuuliziwa maswali mengi, na hivyo itikadi ya Waislamu juu ya huu Ufunuo wa mwisho wa Allah ingelivunjikia mbali na matokeo yake yakawa kwamba Uislamu ungelipoteza nguvu yake.

MMoja wa Alim wa Kishia. Mizra husayn Nouri (aliyefariki mnamo mwaka 1320 Hijiriya)

aliandika kitabu kiitwacho: Faslu'l Khitab ambacho ndani yake, kwanza alizikusanya hadith za Tahriif zote kutoka kwenye vitabu vya Kissuni, kasha akazikusanya Hadithi zote kutoka kwenye vitabuvya kishia akatoa uamuzi wake binafsi kuhusaiana na suala la Tahrif ya Qur'ani ambao ulikuwa kinyume na itikadi ya Kishia ikubalikayo. Mara tu baada ya kitabu hicyo kuchapishwa, mkanusho wake ulichapishwa; na hivyo kitabu hicho kikatolewa thamani yake, kikabakia kwenye kushaulika na kisichofahamika kabisa hata kwenye uwanja wa elimu ya Kishia. Hivi hapa Uislamu wa Kimarikani umekichapisha kitabu hiki Faslu'l Khitab, lakini baada ya kuiondoa sura ya Hadith za Kissuni. Wao hutangaza kuwa kitabu hicho ni "kitabu sahihi cha Kishia" chenye kuthibitisha kwamba Mashia hawaiamini Qur'ani. Kama watu hawa wangalikuwa waaminifu kweli, basi wangelikichapisha kitabu chote; hapo, mabwana zao wangeliweza "kuthibitisha" kwamba Ummah wa kiislamu wote hauiamini Qur'ani.

Malumbano haya ya kujitweza kwetu yangeliwapa Wahubiri wa Kikristo zana bora zaidi za kuutikisia na kuutatarisha msingi wa itikadi ya Waislamu juu ya Qur'ani. Wanategemea kwamba kwa njia hii, Waislamu wengi watashawishika kuukubali Ukristo, na hata wale watakaokataa kuwa Wakristo, hawatasalia kwenye hali ya kuwa Waislamu barabara wala hawangeweza kukifuata kitabu ambacho ussahihi wake unatiliwa shaka.

Mwingereza mmoja aliyekuwa na maarifa ya utawala, aliyeitwa Gladstone anasemekana kwamba safari moja alismama kwenye Bunge la Uingereza huku ameishika nakala ya Qur'ani mkononi mwake, na akatamka kwa sauti kuu akisema; "kwa kadiri Waislamu wabakiavyo kukifuata kitabu hiki, Waingereza hawataweza kuwatisha" . Baada ya kuyasema hayo, Mwingereza

huyu aliwashauri watu wake kuitikisa makri ili kuitikisha itikadi ya Waislamu juu ya Qur'ani.

Maarifa ya kimashambulizi ya Kufr dhidi ya Uislamu yamefaulu huko Uturuki, Misri, Algeria, na nchi nyingine ziitwazo

nchi ya Kiislamu, ambako modeli ;ya Waislamu imeundwa mabayo huonekana kuwa kinyume na Uislamu na Qur'ani. Kundi la aina hii lilikuwa karibuni sana lifaulu huko Iran kwa shukrani za utawala wa Pahlavi. Lakini mipango yao ilishindwa kwa sababu ya viongozi wa kidini chini ya uongozi wa Marehemu Imamu Ayatullah al'Uzma Khomeini na kwa sababu ya uchamungu wa taifa la Iran. Siku hizi maadui wa uislamu wanitumia propaganda hii ya *Tahriif* ili kuifikia shabaha yao hii.

Hayo ndiyo waliyoyapanga lakini Allah Subhanahu wa Taala anasema:

«يريدون ليطفئوا نور الله بأفواههم والله متم نوره ولو كره الكافرون.» سورة الصف آية ٨

"Wanataka kuizima Nuru ya Allah kwa vinywa vyao, na Allah Ataikamilisha Nuru yake ijapokuwa makafiri wakirihike".

(As – Saf, 61:8).